



## Maswali na Majibu

1. Mapaja wa Rebeka, gani alizaliwa kwanza?  
*Esau*
2. Paja gani ndiye Mungu alisema atambariki?  
*Yakobo*
3. Mbona Esau aliuza nafasi ya mzaliwa wa kwanza?  
*Kwa sababu alikuwa na njaa na alitaka kitoweo cha Yakobo. Alipenda vitu vya uzima wa saa hii kuliko ahadi za Mungu.*
4. Yakobo alipataje baraka?  
*Alidanganya Isaka kwamba yeye ni Esau.*
5. Yakobo alipokuwa Betheli aliota eti nini?  
*Aliona ngazi ilioienda mbinguni na malaika waliendea juu na chini.*
6. Yakobo alioa nani alipokuwa akiishi na mjomba wake Labani?  
*Lea na Raheli*
7. Yakobo alikuwa na wana wangapi? Hii ilitimiza ahadi za Mungu namna gani?  
*12. Walikuwa makibili 12 ya Israeli – taifa – watu wa Mungu.*
8. Yakobo alishindani na nani alipokuwa akienda kukutana na Esau? *Malaika*
9. Yakobo alipewa jina gani mpya? Ina maana gani?  
*Israeli. Mkuu wa Mungu.*
10. Malaika alimteguu kiungo cha pacha. Hii ilifunza Yakobo nini?  
*Hakuweza kufanya chochote kwa nguvu zake. Lazima aamini Mungu.*

## Mistari ya kukariri

Mwanzo 28:13 – 14      Mwanzo 28:15      Mwanzo 32:28

## Mazungumzo

Eleza maana ya nafasi ya mzaliwa wa kwanza. Ahadi za mzaliwa wa kwanza zilikuwa na baraka gani?

Soma Malaki 1:2 – 3 na Waembrania 12:16 – 17. Mbona Mungu alimpenda Yakobo na kumchukia Esau?

## Kuandika

Soma Mwanzo 29:14 – 30. Andika vile Labani alimdanganya Yakobo.

## Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

### Somo la 10    Yakobo – Baba wa Waisraeli

**SOMA**    Mwanzo 25:24 – 34; 27:1 – 35; 28:10 – 22; 32:22 – 32


#### SOMO

Isaka alioa Rebeka na alimpenda. Baada ya muda mrefu Rebeka alizaa wana mapaja wawili. Mwana wa kwanza kuzaliwa aliitwa Esau. Na wapili aliitwa Yakobo. Hawa wana wawili walipokua walikuwa tofauti sana kwa hali zote. Esau alikuwa mwekundu na mwili wa unywele. Alipenda kusafiri akiwinda wanyama akikula. Esau alifurahia na kupenda sana hiyo kazi yake ya kuwinda. Yakobo alikuwa na mwili mwororo. Alikuwa mkulima na alipenda kukaa nyumbani akilinda mifugo yao. Yakobo alimpenda Mungu. Alitaka awe na sehemu kwa ahadi za Mungu. Isaka alimpenda Esau zaidi na Rebeka alimpenda Yakobo.

Ahadi zenye Mungu alifanya ni za maana sana. Hizo ahadi za elekeea kwa wokovu na kwa Ufalme wa Mungu duniani. Mungu alipea Ibrahimu hizi ahadi. Baadaye akampa Isaka. Halafu zilipewa kila mwana wa kwanza kwa kila familia. Esau alikuwa **mzaliwa wa kwanza**, kwa hivyo alikuwa na **haki** ya kupata hizo ahadi. Hizi zinaitwa **haki za mzaliwa wa kwanza**. Lakini Mungu alikuwa ameambia Rebeka kwamba mwana mdogo atapata baraka za ahadi.

Siku moja Esau alikuja nyumbani kutoka mawindoni. Alikuwa hajakuwa nyumbani kwa siku nyingi. Alikuwa na njaa, amechoka karibu kuzimia. Yakobo alikuwa anapika kitoweo kitamu. Harufu nzuri ya chakula ilimfanya Esau akawa na hamu ya kukula hicho chakula cha Yakobo. Esau alitaka sana kitoweo cha Yakobo mpaka akakubali kuuza baraka zake za mzaliwa wa kwanza kwa kubadilisha kwa chakula. Esau alipenda vitu vya maisha ya saa hii kuliko ahadi za Mungu. Yakobo alimpenda Mungu na alitaka ahadi za Mungu na wokovu wa maisha yake.

Isaka alipokuwa mzee hakuweza kuona, aliambia Esau aende mawindoni na amletee nyama aliyoipenda. Aliambia Esau kwamba atampa baraka za ahadi za Mungu atakaporudi kutoka mawindoni.



Rebeka alitengeneza kitoweo. Alivaa Yakobo ngozi ya mbuzi ili mwili wake uonekane wa unywele kama wa Esau. Tena akamvalisha nguo za Esau ili awe na harufu ya Esau. Yakobo alidanganya baba yake, Isaka. Isaka alipea Yakobo baraka za ahadi. Esau aliporudi alikasirika sana alipokundua kwamba Yakobo alidanganya baba yao, Isaka. Alimchukia Yakobo sana kwa sababu alikuwa amepewa baraka. Esau alipanga kumuua Yakobo. Yakobo hakutakiwa kudanganya babaye. Mungu alimfundisha Yakobo kwamba uongo ni mbaya, kwa kuititia kwa matokeo mengine kwa maisha yake baadaye.

Yakobo alitorokea kwa jamii yake kule Harani. Alipokuwa njiani, Mungu alimwonekania kwa ndoto. Kwa hizo ndoto, Yakobo aliona ngazi iliyoelekea mbinguni. Aliona malaika wakienda juu na chini kwa hiyo ngazi. Mungu alirudia hizo ahadi zenyenye alikuwa ameambia Ibrahimu na Isaka. Mungu aliaambia Yakobo kwamba atakuwa na wazao wengi. Mungu aliahidi kwamba atampa Yakobo na wazao wake nchi yote. Tena Mungu aliahidi Yakobo atakuwa naye popote aendapo. Alimwambia kwamba siku moja atarudi na kuishi kwa nchi ya Kanaani aliyoleta ameahidi.



Alipofika Harani aliishi na mjomba wake Labani. Yakobo alichunga kondoo wa Labani. Yakobo alioa wasichana wawili wa Labani – Lea na Raheli. Labani alimdanganya Yakobo mara nyingi. Lakini Mungu aliendelea kumbariki. Yakobo alijifunza kwamba kudanganya watu ni mbaya sana. Yakobo alikaa Harani kwa miaka 20. Wakati huo wanawe kumi na wawili walizaliwa.

Baadaye, wana kumi na wawali wa Yakobo ndio walikuwa khabila kumi na mbili. Ndio walikuwa khabila kumi na mbili za Israeli. Baadaye hizi khabila kumi na mbili zilikuja zikawa khabila za nguvu sana. Hivi ndio Mungu alikuja kutimiza ahadi yake kwa Ibrahimu, Isaka na Yakobo kwa kukuwa taifa kubwa.


Baada ya hizo miaka ishirini Yakobo aliamua kurudi nyumbani kwa nchi ya Kanaani. Alikuwa bado anauoga kwa nduguye Esau. Alipokuwa njiani alisikia kwamba Esau alikuwa anakuja kumlaki na watu 400. Yakobo aliogopa sana. Aliomba Mungu amuokoe yeye na familia yake.

Malaika alimkuja Yakobo. Yakobo alimuuliza malaika ambariki. Yakobo alishindana na malaika usiku kucha akitaka kubarikiwa. Hakuwachilia malaika aende mpaka awe amembariki. Kulipofika alfajiri, malaika alimgusa paja na likaumia kwa kiungo. Hii ilizababisha Yakobo kuchechemea. Hii ilikuwa funzo kwa Yakobo kwamba hawezি kutumia nguvu zake – Ilikuwa vigumu yeye kupigana na Esau hali ana mguu mbaya. Ilimfunza kwamba lazima aamini Mungu wakati wa shida. Hata nasi lazima tuamini Mungu wakati kuna shida.



Ilipofika asubuhi, malaika alimpa Yakobo baraka. Alibadilisha jina la Yakobo na kumuita **ISRAELI**. ‘Israeli’ maana yake ‘mkuu wa Mungu’. Familia ya wana kumi na wawili wa Yakobo ndio taifa la Israeli na baadaye nchi ya Kanaani iliiwtwa Israeli. Jina Israeli ndilo jina lililopewa taifa na nchi yenye Mungu aliahidi Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Hili jina lilionyesha kwamba ahadi za Mungu zilikuwa zinatimizwa. Ibrahimu, Isaka na Yakobo ni baba wa taifa kubwa lenye Mungu aliahidi.

Yakobo alikutana na Esau. Hakukuwa na hasira yejote. Mungu alikooa Yakobo na familia yake kutoka kwa Esau. Esau alienda kuishi kwa nchi ya Edomu. Yakobo na familia yake walienda kuishi kwa nchi ya Kanaani. Wakati huu inaitwa nchi ya Israeli. Ni nchi yenye Mungu aliahidi wazao wa Ibrahimu. Wana 12 wa Yakobo ndio taifa la Israeli. Mungu huwa anatimiza ahadi zake.



Reuben Simoni Levi Yuda Isakari Zabuloni Dani Naftali Gadi Asheri Yusufu Benyamin

**Khabila kumi na mbili za taifa la ISRAELI**